JINA:.................................................................................... NAMBARI:.......................

SHULE:.................................................................................. SAHIHI:............................

TAREHE:.........................

For More Free KCSE Past papers Visit www.freekcsepastpapers.com

102/2
**KISWAHILI**
KARATASI YA 2
**(LUGHA)**
JULAI/AGOSTI - 2014
**MUDA: SAA 2 ½**

# TATHMINI YA SHULE ZA UPILI ZA JIMBO LA MERU - 2014

*Cheti cha Kuhitimu Elimu ya Sekondari Kenya.*

102/2
**KISWAHILI**
KARATASI YA 2
**(LUGHA)**
JULAI/AGOSTI - 2014
**MUDA: SAA 2 ½**

**MAAGIZO**

a) Andika jina lako na namba yako katika nafasi zilizoachwa hapo juu.
b) Jibu maswali yote
c) Andika majibu yako katika nafasi zilizoachwa katika kitabu hiki cha maswali

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 3 | 40 | |
| 4 | 10 | |
| ALAMA | 80 | |

*Karatasi hii ina kurasa 12 zilizopigwa chapa.*
*Mtahiniwa ahakikishe kuwa kurasa zote za karatasi hii ya mtihani zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.*

## 1. UFAHAMU – (ALAMA 15)

For More Free KCSE Past papers visit www.freekcsepastpapers.com

Ripoti ya Shirika la New World Wealth ilipasua mbarika kuhusiana na hali halisi ya uchumi wa Kenya na dhuluma zake. Kwenye ripoti yake shirika hili lenye makao yake mjini London nchini Uingereza lilisema kuwa watu 8200 wanamiliki asilimia 62 ya pato la taifa letu.

Ripoti hii iliweka wazi kuwa mabwanyenye hawa wenye ukwasi wa kupatia mtu kichaa wana sifa mbili kuu. Kuwa wana mizizi madhubuti kwenye jukwaa la siasa za Kenya. Aidha, wanamiliki bahari za mashamba huku wengine wakimiliki maekari ya ardhi sawa na uliokuwa mkoa wa Nyanza. Kimsingi ripoti hii imeshadidia ukweli kuwa pengo baina ya maskini na matajiri nchini Kenya limefika kiwango cha kulipuka. Wakati mamilioni ya wakenya wanalazimika kuishi kwa mlo mmoja tu kwa siku, mabwanyenye wamechimbia mamilioni ya dola kwenye benki Ulaya.

Wakati mamilioni ya wakenya wanaishi kwenye mabanda ya **mbavu za mbwa**, wakwasi wetu wanapiga ramli kuamua ni kasri lipi watalala jioni baina ya msururu mrefu wa makasri wanayomiliki. Wakati maskwota wanalala kwenye lindi la bahari la chawa, wakwasi nao wanajenga **viramba mawingu** kwenye miji mikuu kwa wepesi wa kuku kumeza punje la nafaka.

Ndugu msomaji hebu weka kwenye mizani ya akili zako kuwa kigogo wa kampuni ya Bidco anakadiriwa kuwa na utajiri unaozidi jumla ya mabilioni ya pesa zilizotolewa na serikali kuu kwa serikali za kaunti zote nchini. Hii ni hali halisi ambayo serikali ya Kenya haina budi kuweka misingi ya kurekebisha. Ama haingii akilini mwa wataalamu wa kiuchumi kutoa takwimu kila mwaka kuonyesha kasi ya ukuaji uchumi ikiwa mamilioni ya wakenya wanazidi kuishi chini ya mstari wa kipato cha dola moja kwa siku. Ni kinaya kusema kuwa pato la jumla la taifa lilikuwa kwa kiasi hiki au kile iwapo zaidi ya wakenya 1.7 milioni wanakabiliwa na baa la njaa.

Ustawi wa taifa hauwezi kuelezwa kwa sehemu ndogo ya viongozi matajiri wanaozidi kuhodhi utajiri wa kupindukia. Huku mamilioni ya wakenya wakiwa hawamudu mahitaji ya kimsingi ya maisha. Ukuaji uchumi endelevu unafaa kuainishwa na kuwepo kwa mfumo wazi wa kusambaza uwezo wa kiuchumi kwa wakenya wote.

**Maswali**

(a) Yape makala anwani mwafaka (alama 2)

..................................................................................................................

..................................................................................................................

(b) Eleza sifa mbili zinazowatambulisha mabwanyenye. (alama 2)

..................................................................................................................

..................................................................................................................

..................................................................................................................

..................................................................................................................

For More Free KCSE Past papers Visit www.freekcsepastpapers.com

(c) Linganisha maisha ya bwanyenye na mtu wa kawaida kwa mujibu wa ripoti hii. (alama 4)

(d) Dhibitisha kuwepo kwa pengo la kustaajabisha kati ya wakwasi na watu wa kawaida kwa kuzingatia kifungu. (alama 3)

(e) Eleza jinsi uchumi wa taifa unaweza kustawishwa kwa mujibu wa kifungu. (alama 2)

(f) Eleza maana ya vifungu vifuatavyo (alama 2)

(i) Mbavu za mbwa

(ii) Viramba mawingu

(ALAMA 15)

Ajira ya watoto ni tatizo sugu linalokumba ulimwengu wa sasa, hasa katika nchi zinazoendelea. Jambo la kusikitisha ni kwamba hivi ndivyo ilivyo, katika nchi nyingi za ulimwengu huu. Kuna idadi kubwa ya watoto wanaoajiriwa katika nyanja mbalimbali za jamii. Zoipo sababu nyingi zinazowasukuma watoto kutafuta ajira barani Afrika, kwa mfano, familia nyingi huishi maisha ya kifukara hivi kwamba kushindwa kuyatimiza mahitaji muhimu hususan watoto. Kupanda kwa gharama ya maisha kunazidisha viwango vya umaskini. Ukosefu wa lishe bora pia huwafanya kutoroka nyumbani kutafuta ajira. Janga la UKIMWI limesababisha kuwepo kwa idadi kubwa ya mayatima wanaoishia kutafuta ajira ili kuyakimu maisha. UKIMWI umezifanya familia nyingi kuwaondoa watoto shuleni ili waweze kuajiriwa kwa lengo la kuinua pato la familia hizo.

Wengine hujiingiza katika vitendo vya jinai wanapokosa ajira. Huchukua sheria mikononi mwao, wakaendeleza vitendo vya ukatili kama vile kuwahangaisha watu na kupora mali yao au hata kuwakaba roho. Aidha wengine kujikuta kwenye madanguro ambako huendesha biashara haramu.

Uundaji wa umoja wa Afrika hivi majuzi ni hatua muhimu ya kushughulikia matatizo ya Afrika kama vile ajira ya watoto, kuzorota kwa miundo msingi, magonjwa, njaa, umaskini, ufisadi na ukabila. Katika kushughulikia hali za watoto, nchi za Afrika hazina budi kuzingatia masharti yaliyowekwa kwa umoja wa mataifa kuhusu haki za watoto. Nchi nyingi za Afrika ziliidhinisha mkataba wa masharti hayo ikiwemo nchi ya Kenya. Nchi hizi basi lazima zishughulikie haki za watoto kupitia sheria za nchi. Watoto ni raslimali muhimu na ndipo tumaini la kuwepo kwa kizazi cha baadaye.

Maswali

(a) Eleza mambo muhimu yanayozungumziwa katika aya ya kwanza.(Maneno 50-55)(Alama 7)

Matayarisho

...........................................................................................................................

...........................................................................................................................

...........................................................................................................................

...........................................................................................................................

...........................................................................................................................

...........................................................................................................................

...........................................................................................................................

...........................................................................................................................

...........................................................................................................................

...........................................................................................................................

...........................................................................................................................



For More Free KCSE Past papers Visit www.freekcsepastpapers.com

Jibu

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

For More Free KCSE Past papers Visit www.freekcsepastpapers.com

(b) Fupisha aya mbili za mwisho. (Maneno 50 – 55) (Alama 6)

**Matayarisho**

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

**Jibu**

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

3. MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

(a) Fafanua sauti zifuatazo: (al.2)

(i) Ghuna

..............................................................................................................

..............................................................................................................

(ii) Sighuna

..............................................................................................................

..............................................................................................................

(b) Tofautisha baina ya kiimbo na shadda. (al.2)

..............................................................................................................

..............................................................................................................

..............................................................................................................

..............................................................................................................

(c) Ainisha maneno katika sentensi. (al.2)

Haw. wawili ni ndugu

..............................................................................................................

..............................................................................................................

(d) Tunga sentensi ukitumia kitenzi -fa katika kauli ya kutendewa. (al. 2)

..............................................................................................................

..............................................................................................................

..............................................................................................................

..............................................................................................................

(e) Sahihisha kwa namna mbili. (al. 2)

Hapa kunapendeza sana

..............................................................................................................

..............................................................................................................

(f) Andika kwa ukubwa (al. 2)

Meza hii ndogo ina uchafu

..............................................................................................................

..............................................................................................................

(g) Eleza matumizi mawili ya mshazari (/). (al 2)

..............................................................................................................

..............................................................................................................

(h) Kanusha (al. 2)

Ningeenda sokoni ningenunua mboga

..............................................................................................................

..............................................................................................................



For More Free KCSE Past papers Visit www.freekcsepastpapers.com

(i) Changanua kwa kielelezo cha matawi. (al. 4)

Mchezaji aliyefunga bao amepanda jukwaani.

For More Free KCSE Past papers Visit www.freekcsepastpapers.com

(j) Tunga sentensi katika hali ya mazoea. (al. 2)

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

(k) Andika kinyume (al. 2)

Babu mnene anatembea haraka

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

(l) Eleza matumizi mbalimbali ya 'ni' katika sentensi hii. (al. 2)

Niambie ni wapi kumeandaliwa mkutano.

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

(m) Tambua na ueleze aina za yambwa. (al. 2)

Washindi walituzwa zawadi.

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

(n) Tumia 'O' rejeshi tamati katika sentensi. (al. 2)

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

(o) Andika katika usemi halisi. (al. 3)

Mutwiri alimwambia kwamba angeenda kumjulia hali siku iliyofuata.

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

(p) Tambua kirai husishi na kirai kiwakilishi katika sentensi ifuatayo. (al. 2)

Hawa wote walisimama kando ya barabara.

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

(q) Eleza maana tatu zinazojitokeza katika sentensi. (al. 3)

Mama alimwendea mtoto wake

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

(r) Tafsiri msamiati ufuatao kwa lugha ya Kiswahili. (al. 2)

(i) Laptop

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

(ii) Devolution

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

For More Free KCSE Past papers Visit www.freekcsepastpapers.com

4. ISIMU JAMII ALAMA 10

(ii) Eleza nadharia tatu zinazoeleza chimbuko la lugha ya Kiswahili. (al. 6)

For More Free KCSE Past papers Visit www.freekcsepastpapers.com

(b) Eleza maana ya Istilahi zifuatazo kama zinavyotumika katika isimu jamii. (al. 4)

(i) Lugha sanifu

................................................................................................................................

................................................................................................................................

(ii) Lahaja

................................................................................................................................

................................................................................................................................

(iii) Uwili lugha

................................................................................................................................

................................................................................................................................

(iv) Lafudhi

................................................................................................................................

................................................................................................................................

For More Free KCSE Past papers Visit www.freekcsepastpapers.com